From Revival Ministries Australia
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

******OKTOBA2020****OKTOBA2020****OKTOBA2020****OKTOBA2020******

KRISTO JUU YA YOTE - ukweli wa ushindi

Wengi wanahusika na eskatolojia[uchunguzi wa siku za mwisho].Wanadamu wanafuatilia mafundisho na maelezo fulani ya yale yatakayotokea duniani katika enzi yetu. Wengi wanatabiri na kufasiri matukio ya 'kiasili',hata hali ya saa hii ya korona. Hata hivyo, Bibilia iko wazi sana - kwamba vitu vyote vimo ndani ya Kristo na Kristo ndiye ushindi wa kanisa katika mataifa. Tunaweza 'kusimama na kuhimili' (Waefeso 6:12).

Mungu ameniongoza, mimi Paulo, kuanzisha mfululizo wa mafundisho yenye mada 'Ukweli wa ushindi'. Fundisho hili linaanza na kila wiki ninaweza kushiriki fundisho linalofuata si tu hapa Shiloh Centre, bali pia kwa mataifa kupitia Zoom. Tayari tunapokea majibu ya wandugu kuachiliwa kutoka kwa kushindwa na nguvu za kipepo, sote tunapoangalia tena upya ukweli wa ushindi ndani ya Yesu Kristo.

Tutachunguza yale ambayo kwa wengi yatakuwa Maandiko ya 'kawaida', lakini tunataka kufahamu kikamilifu kwa Roho na kushika kwa Roho neno la Mungu ambalo linatuambia kuhusu ushindi kamili wa Yesu aliye Kristo kupitia kwa kifo chake, kuzikwa na kufufuka. Tunafaa kutangaza huo ushindi! Hii ndiyo injili!

OMBI LA PAULO KWETU

Paulo anatuombea katika Waefeso 1:17-19a [lakini kwa kweli ombi hilo linaendelea hadi mwisho wa sura hiyo].Ombi ni kwamba "Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu ,awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye [Bwana Yesu],macho ya mioyo yenu yatiwe nuru,mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo".Kuna mambo mengi muhimu katika ombi hili la ajabu na tunaombewa! Tunaweza kushika ombi hili kwetu sisi leo na limekuwa nuru kubwa na nguvu katika maisha yangu kwa miaka mingi.

- Paulo anamwomba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo,Baba wa utukufu
- Paulo anamwomba Mungu ili awape[au awajalie] roho ya hekima na ufunuo,
- Hii roho ya hekima na ufunuo iko katika kumjua Yeye,ambayo katika muktadha,ni ufahamu wa Yesu Kristo. Neno 'ufahamu' ni 'epignosis', kumaanisha 'kutambua kwa kupambanua kikamilifu'. Mungu anataka tujue Yesu ni nani,na tunaweza tu kumjua kwa ufunuo. Petro alipitia hii katika Mathayo16:15-18. Alitambua kwa upambanuo kamilifu kwamba huyu Yesu wa Nazareti ndiye kweli Masiha, Mwana wa Mungu aliye hai!

Mambo matatu kufahamu

Paulo anaombea macho ya mioyo yetu yatiwe nuru, ili tuweze kujua:

i. tumaini la mwito wake jinsi lilivyo
ii. utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo,

iii. na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio

Kila moja kati ya hivi vitu vitatu ambavyo Paulo anataka tutiwe nuru kufahamu, ni uchunguzi kwa kipekee. Tunataka kuchagua 'ukuu wa uweza wake'. Mungu anataka tujue ukuu wa uweza huu ili tuweze kuwekwa vizuri kama sehemu ya mwili wake.

> Neno 'uweza' ni neno la Kigiriki 'dunamis' kurejelea uweza usio wa kawaida wa Mungu. Kisha msitari wa 19 wa Waefeso 1 linaendelea kusema kwamba uweza huu "kwetu sisi tuaminio". Ni "uweza wake mkuu".
> Hili neno kwa 'uweza' ni 'kratos'na kimsingi linarejelea mamlaka ya ufalme wa Mungu, utawala na ukuu [angalia Word Wealth kwa 1Timotheo"
> 6:16 katika Spirit Filled Life Bible NKJV]. Ni kusudi la Mungu kuachilia uweza wake kwetu. Ameamua hii kwa mamlaka yake.

Mungu amefanya "Uweza wake mkuu ndani ya Kristo"alipomfufua kutoka kwa wafu (Waefeso 1:20). Huu uweza mkuu unao ndani yake nguvu za ufufuo. Hallelujah!

Huu uweza mkuu "ulimketisha yeye[Kristo] kwenye mkono wake wa kuume katika sehemu za kimbinguni". Kristo kutoka wakati wa kufufuka kwake alipokelewa katika sehemu za kimbinguni na kuketishwa katika mahali juu zaidi na mamlaka yote "mkono wake wa kuume".

Mkono wa kuume

Marejeleo kwa 'mkono wa kuume' ni pale mahali pa mamlaka na uweza, na ona kwamba Kristo "ameketi". Wafalme na Malkia huketi wanapotawala, wakitoa hukumu na amri na yale yote ambayo mtawala mkuu hufanya. Tunaweza kusema kwamba haiwezekani 'kumwondoa'Kristo. Ni muhimu kuelewa hii, tunapoanzisha 'ukweli wa ushindi',na ushindi uko katika Kristo ,kujua yeye ni nani na kujua "ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio"

· Marko 16:19 inasema kwamba Yesu "akachukuliwa juu mbinguni ,akaketi mkono wa kuu kuume." Kutoka wakati huo wanafunzi "wakatoka wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao,na kuthibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo".

· Zaburi 110:1 inasema kwamba Masiha alikuwa "Uketi mkono wangu wa kuume , Hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako".
Nukuu hii hutambulika mara nyingi katika Agano jipya na ni neno la unabii muhimu sana la Agano la Kale kuhusu uongozi.

· Waebrani 10:12-13 inasema "Lakini huyu ,alipokwisha kutoa kwa ajilia ya dhambi zetu dhabihu moja idumuyo hata milele ,aliketi mkono wa kuume wa Mungu,tangu hapo akingojea hata adui zake wakwe kuwa chini ya miguu yake". Hii ilikuwa ni matumizi na utimizo wa Zaburi 110.

Kuketishwa juu zaidi

Kristo aliketi "juu sana kuliko ufalme wote [SC#746/utawala/watawala uweza [mamlaka-Gk.#1849 'exousia'] na nguvu [SC# 1411 uweza] na utawala [SC#2963 ubwana] na kila jina litajwalo, si tu kwa enzi hii bali pia kwa ile inayokuja" Waefeso 1:21.

Andiko hili linafunua kwamba kuna maeneo ya kazi za kipepo kuanzia kiwango cha juu sana cha mamlaka ya kipepo[falme] hadi kile cha 'kila jina',kurejelea kila aina ya ibada ya sanamu ya vitu vilivyoundwa na mbao na jiwe na ibada kutokana na sehemu kubwa watu.
Kwa mfano, zaidi ya watu bilioni moja huabudu Allah ya Waisilamu; kama vile wengi wanaabudu miungu ya wa Hindu na Krishna kama moja ya miungu yao mkuu; na Buddha ina ibada iliyosambaa.

Habari njema ya injli ni kwamba Yesu Kristo ameketi katika mamlaka juu sana! Ni muhimu kwa sisi sote katika mwili wake kanisa, kufahamu na kujua "ukuu wa uweza wake kwetu sisi tuaminio"(Waefeso 1:19).Hii ni muhimu kwetu sisi kujua na kufahamu ukweli wa ushindi.

Yesu ndiye kichwa juu ya yote

Mungu "amevitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa"(Waefeso 1:22). Kupitia kifo chake, kuteremka kwake kuzimu [Gehena] na kufufuka kwake, Yesu "amefanywa Bwana na Kristo" (Matendo 2:36). Ame "Inuliwa [inuliwa kwa mahali pa juu] kwenye mkono wa kuume wa Mungu". Alipokea "kutoka kwa Baba ahadi ya Roho Mtakatifu, [na] akamwaga" Roho Mtakatifu (Matendo 2:33). Yesu tayari alikuwa ameinuliwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu kwa kufikia wakati alimwaga Roho Mtakatifu siku ya Pendekote.

Kristo alipofufuliwa kutoka kwa wafu, "aliketishwa kwenye mkono wa kuume" (Waefeso 1:20). Yesu amefanywa kuwa kichwa juu ya vitu vyote. Katika muktadha huo, 'vitu vyote' ni nini? Msitari wa 21. umetuambia: ni "falme na mamlaka na nguvu na utawala na kila jina".

Wakolosai 2:15 inatuambia kwamba Yesu "alizivua enzi na mamlaka,nakuzifanya [enzi na mamlaka] kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo".Hii ndiyo habari njema ya injili! Injili na ya ushindi na kupitia kuhubiriwa kwa injili ya ushindi mkuu wa Yesu Kristo, ukweli wa ushindi unafanywa kujulikana na kupitiwa na mwili wake.

Yesu aliye Kristo ndiye Bwana wa mabwana na Yesu Kristo ndiye Mfalme wa wafalme, Mfalme aliyepakwa Mafuta (Ufunuo 19:16). Yesu alifanywa awe kichwa juu ya vyote kupitia kwa ushindi wa msalaba kabla kupewa kwa kanisa, ambalo ni mwili wake, kuwa kichwa juu ya kanisa. Yesu alikuwa Mfalme anayeshinda ambaye aliketi chini kwenye mkono wa kuume wa Mungu [kwenye kiti chake cha enzi- Ufunuo 3:21].

Yesu ndiye kichwa cha kanisa

Kama "Kichwa juu ya vitu vyote" na adui wake wote "chini ya miguu yake", Kristo alitolewa kama "kichwa juu ya vitu vyote kwa kanisa" (Waefeso 1:22). Kichwa cha kanisa ni Mfalme mshindi anayetawala ambaye ameshinda adui zake wote na ambaye amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani (Mathayo28:18).

Akiisha kutolewa kwa kanisa kama kichwa na kutambua na kufahamu kwamba kanisa ni mwili wake ambalo kwalo Kristo anaenda "kujaza yote kwa yote",tunaanza kuona kwamba ukweli wa ushindi ni kupitia kuwa na "macho ya mioyo yetu kutiwa nuru kujua…ukuu wa uweza wake kwetu sisi tuaminio" (Waefeso 1:19).

Kanisa litajaza vitu vyote

Yesu anajaza,na atajaza kikamilifu ulimwengu [vitu vyote] na ukamilifu wake (Waefeso 1:23). Anafanya hii na atakamilisha hii kupitia kwa mwili wake, kanisa. Kanisa ndilo mwili-mwili ulio na sehemu nyingi (1 Kor.12:12) -uliopangwa na kutayarishwa kufanya kazi, likijengwa kupitia huduma tano ambazo Mungu ametoa (Waef.4:11).

- Huu mwili umekuja kwa umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu.

- Huu mwili umekuja kuwa mtu mkamilifu,kufikia kwenye cheo kimo cha utimilifu wa Kristo (Waefeso 4:13).

- Huu mwili haujaundwa tena na watoto ambao wanatupwa huku na huku "kila upepo wa elimu" bali wamewekwa thabiti katika imani na kumjua Mwana wa Mungu.

- Hili ndilo kanisa ambalo linakua katika yote, katika yeye aliye kichwa-Kristo (Waef.4:15b).

- Hli ndilo kanisa ambalo litafanya kazi katika ukomavu wote na "kila kiungo kikisaidia …kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja".

- Hili ndilo kanisa ambalo limejawa,na linafanya kazi,katika upendo wa 'agape'.

Tunapokua katika hili kanisa, tunakua katika ufahamu wa ukuu wa uweza wake kwetu sisi tuaminio. Huu ndio ufahamu ambao hufunua kwetu

Ukweli wa ushindi.

Paul Galligan.